

Jamii ifanye nini ili kuondoa unyanyapaa kwa wagonjwa wa TB?

Jamii lazima ifahamu yafuatayo:

- Kwamba vimelea nya TB huenea kwa njia ya hewa kutoka kwa mgonjwa kwenda kwa mtu mwingine
- TB inatibika na kupona kabisa
- Mgonjwa wa TB aliyeanza matibabu hawesi kuambukiza watu wengine
- Mgonjwa TB asipotumia dozi kwa usahihi husababisha usugu wa vimelea kwa dawa za kutibu TB
- Matibabu ya TB ni miezi sita hadi kumi na mbili (kulingana na aina ya kifua kikuu)
- Matibabu ya TB yanapatikana bila malipo katika vituo vyote nya kutolea huduma nya serikali na nya binafsi.
- Kutowatenga wagonjwawa TB wakishaanza matibabu
- Kuwapa ushirikiano na upendo ili kuwasaidia waweze kukamilisha matibabu na kuepuka usugu.

HITIMISHO

Unyanyapaa unasababisha kuendelea kuenea kwa maambukizi ya TB katika jamii yetu na kutokuwa na matokeo mazuri ya matibabu kwa wagonjwa.



Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,
Jinsia, Wazee na Watoto



**KUMBUKA:
TB inatibika bila malipo**

Kwa maeleo zaidi wasiliana na
mtohuduma wa / za Afya aliye karibu nawe.

Kimetolewa na:

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,
Wazee na Watoto

kupitia

Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua

Kikuu na Ukomaa

S.L.P. 9083, Dar es Salaam, Tanzania.

Barua pepe: info@moh.go.tz,

Tovuti: www.ntlp.go.tz,

Toleo la 2016

**EPUKA
UNYANYAPAA
DHIDI YA
MGONJWA WA
KIFUA KIKUU**



UTANGULIZI

Unyanyapaa ni hali ya kumdharaau au kumtenga mtu kutokana na tatizo la kiafya alilo nalo. Watu wenyematatizo ya maradhi kama vile ukoma, TB na virusi vya UKIMWI, wamekuwa wakitengwa, kudharauliwa au kunyooshewa vidole na familia pamoja na jamii inayowazunguka. Aidha unyanyapa unaweza kutokea kwa mtu binafsi kwa kujidharau, kujitenga na kuionna hafai mbele ya jamii.

Unyanyapaa unasababisha wagonjwa wa TB kuogopakujitokeza mapema kwa vipimo na tiba na kwa aliyekwishaanza matibabu kukatisha. Hali hii inachangia mgonjwa wa TB kuendelea kuambukiza jamii inayomzunguka.

Kuna aina nyingi za unyanyapaa

- Baadhi ya wagonjwa wenye maambukizi ya TB wanajilaumu na kujitenga kutokana na kunyanyapaliwa na jamii. Wanakubali aibu na lawama zinazotolewa na jamii.



Unyanyapaa wa mtu binafsi

- Unyanyapaa kutoka kwa familia kwenda kwa mgonjwa
Hali hii hutokana na hofu ya kuambukizwa ugonjwa wa TB hivyo kuwepo kwa hali ya kumtenga mgonjwa katika masuala yote ya kifamilia. Mgonjwa anatengewa chumba cha kulala pamoja na vyombo vya chakula.



Unyanyapaa wa familia kwa mgonjwa

- Unyanyapaa toka kwa jamii na uongozi kwenda kwa mgonjwa na familia yake. Jamii inawatenga na kuwanyoshea vidole familia, inasengenya, inawatarania, hawashirikishwi katika shughuli za kijamii kama vile vikao vya mitaa, sherehe pamoja na kupewa taarifa za matukio mbali mbali yanayotokea katika eneo lake.
- Unyanyapaa kutoka kwa wahudumu wa Afya kwenda kwa mgonjwa

mhudumu wa afya na mgonjwa kuhusu tatizo alilonalo. Baadhi ya wahudumu wanatumia lugha mbaya kwa wagonjwa

Sababu zinazosababisha kuwepo kwa unyanyapaa ni :

- Ukosefu wa elimu kuhusu TB jinsi kinavyoambukiza, uhusiano wake na virusi vya UKIMWI, ugunduzi na matibabu
- Kuhuishwa na hali fulani zinazonyanyapaliwa kama vile virusi vya UKIMWI, umasikini, na utumiaji wa madawa ya kulevyo
- Wagonjwa wa TB mara nyingi wanaonekana kuwa hawakuwa makini katika kujikinga
- Ukosefu wa vifaa vya kujikinga kwa wahudumu wa afya na wengine walio katika hatari ya kuambukizwa.

Athari za unyanyapaa

- Wagonjwa wanakuwa na huzuni, upweke, wasiwasi, sonona, kutokujiamini, kukata tamaa, kutaka kujiua au kuingia kwenye ulevi wa kupindukia
- Usiri mkubwa/kujificha na kuzuia watu wasitoe taarifa kuhusu hali yake
- Kuchelewa kufanyiwa uchunguzi / Vipimo na tiba na hivyo kuendelea kueneza ugonjwa wa TB katika jamii na kusababisha vifo
- Kutokumaliza tiba kwa usahihi. Hii inaweza kusababisha usugu wa dawa.
- Wagonjwa wa TB kukosa huduma muhimu katika jamii.